
Kijitabu kwa Mwezeshaji

# Himaya za Maisha

**Kijitabu kwa Mwezeshaji**

Mfululizo wa filamu za watu wa Asili



















Tembelea tovuti **www.lifemosaic.net/eng/tol/more/swahili-version-himaya-za-maisha/** ufahamishwe zaidi kuhusu rasilimali, takwimu na utafiti kuhusu kila aina ya hizi filamu.



# YALIYOMO

**Kuhusu Himaya za Maisha** 6

**Fanya Onyesho** 8


**Maelezo kuhusu filamu**

**Kanda 1 - Vitisho na Haki**
- Utangulizi 12
- Upokonyaji wa Ardhi 13
- Mbinu za Kampuni 14
- Umuhimu wa Himaya 17
- Haki za Ardhi 19

**Kanda 2 - Suluhusho na Msukumo**
- Mpango wa Maisha 21
- Wanawake Mashujaa wa Ololosokwan 23
- Hekari nusu Milioni za Matumaini 26
- Mawasiliano 28
- Utumiaji wa Sheria 29

**Maelezo ya Ziada** 30

# Kuhusu Himaya za Maisha






## Himaya za Maisha ni Nini?

Vifurushi vya Himaya ya Maisha vinatolewa kutumika bure kwa maelfu ya jamii tofauti duniani kote ambako himaya yao zinaongozwa kwa mtindo wa maisha yao ya kijamii.

## Himaya za Maisha ni ya Kina Nani?

Vifaa vya Himaya ya Maisha vinashirikishwa bure kwa maelfu ya jamii tofauti tofauti dunia nzima ambao himaya zao ni muhimu katika maisha yao.

**Himaya za Maisha ni ya:**
Jamii zinazokabili Miradi mikubwa ya kimaendeleo; Jamii ambazo tayari zimekwishapoteza baadhi ama maeneo yao yote na jamii ambazo zimemilikishwa hati miliki ZA himaya zao.

Filamu hizi pia ni nyenzo za kujenga uwezo wa mwashirika yasiyo ya kiserikali na mashirika mengine ya kijamii.

Filamu hizi pia zinaweza kuonyeshwa kwa maafisa wa serikali na watu wengine ambao wanahusika au wanaweza kuathiri watu asili na misitu, pia mashuleni, vyuo vikuu na sehemu nyingine za matukio ya uma.

# Fanya Onyesho

## Kwa nini kufanyika maonyesho ya Himaya za Maisha?

Kushirikisha hadithi, uzoefu na mitazamo baina ya jamii kadhaa, na kusaidia kutoa changamoto za majadiliano yao.

Kujifunza kutokana na uzoefu, mapambano na mbinu za wana jamii asili diniani kote.

Kuelewa kwa undani zaidi kimataifa juu ya unyakuzi wa ardhi na athari zake ratika jamii.

Kupata nguvu kutoka kwa mifano mizuri ya jamii kuandaa kujenga umoja na kupangilia mipango ya baadae.

## Jinsi ya kutumia Himaya za Maisha.

Filamu zaweza kuonyeshwa moja baada ya nyingine, na kila Filamu ifuatwe na majadiliano kaika jamii kuhusu yaliyomo.

Ili kupata matokeo ya juu, maonyesho yanaweza kupewa kusaidiwa na waelekezaji katika jamii wakiwa katika mikutano au kongamano, au wakiwa katika mchakato wa muda mrefu katika uamuzi kwa kibinafsi wa kimaendeleo.

Kila filamu katika hizi za **Himaya za Maisha** inaonyesha mijadala tofauti, hivyo unaweza kuchagua mjadala ambao unawiana na changamoto zinazohusu jamii yako.

Tembelea tuvuti **www.lifemosaic.net/eng/tol/more/swahili-version-himaya-za-maisha/** ufahamishwe zaidi kuhusu rasilimali, takwimu na utafiti kuhusu kila aina ya hizi filamu.



## Jukumu la Mwelekezi wa Jamii

Mtu atakayeilekeza jamii kuhusu himaya ya maisha anaweza kutoka katika jamii inayozumngumziwa, au akatoka shirika lisilo la kiserikali la kwenye shina, au akatoka shirika la kijamii pia anaweza kuwa muelimishaji au mwalimu.

Mwelekezaji asiye mtu anayeweza kufaidika kibinafsi kutokana na maendeleo ya yaliyopendekezwa.


Mwelekezaji huyu ana majukumu yafuatayo; Kutayarisha uonyeshaji wa filamu, kutoa utangulizi wa filamu, kutoa maelekezo katika majadiliano baana ya maonyesho ya filamu na kutoa usaidizi katika mapendekezo yaliyokubalika baada ya onyesho.

## Njia ya Kuandaa maonyesho

Pata ruhusa kutoka kwa jamii na wanajamii.

Fikiria namna watu watakavyoalikwa ukizingatia wanawake, vijana na jamii zingine kutoka maeneo hayo yatayofanyika majadiliano ya maonyesho ya filamu ya jamii husika. Au andaa mikutano maalumu ya hivyo vikundi.

Hakikisha una vifaa sahihi. Utahitaji mashine kwa matumizi ya kanda za filamu na dvd, televishen na spika ili maonyesho yaweze kusikika vizuri. Pia unaweza kuhitaji kifaa cha kukuza taswra (projector) ili kuwezesha watazamaji kuona pasipo shida.



## Ujuzi wa Mwelekezi wa Jamii

Kabla ya maonyesho ya filamu kwa jamii: Tafadhali hakikisha unajua filamu zote. Amua ni filamu gani zinahusika na hali ya jamiiunapofanya maonyesho. Kisha tazama filamu ulizo amua kuwaonyesha wanajamiiili uwe na ufahamu wa yatakayoonyeshwa kabla tukio.

Kama jamii inakumbana na miradi mikubwa ya maendeleo,utafanya maonyesho ya filamu Upokonyaji wa Ardhi, Mbinu za Kampuni ama Wanawake Mashujaa wa Ololosokwan.

Kama jamii bado haina haki ya mashamba,na/ama wanapewa haki katika mikataba au vyeti vya kibinafsi itakua vizuri kuonyesha filamu za Haki za Ardhi.

Kama jamii ina maono ya maendeleo ya muda mrefu katika maeneo yao tafadhali onyesha filamu ya Mpango wa Maisha.

**Wakati wa Maonyesho.**
Maonyesho ya filamu nyingi katika kikao kimoja inachosha na haitakupa muda wa majadiliano. Maonyesho ya filamu moja ama mbili katika mkutano mmoja yaweza kuwa na matokeo mazuri. Katika kila filamu yapaswa uache angalau muda wa saa moja kwa ajili ya majadiliano. Waweza pia kuandaa maonyesho zaidi ya kikao kimoja, ama zaidi ya jioni moja.

Wezesha majadiliano baada ya kuonyesha kila filamu, andaa maswali mapema.



Kwa kila filamu kuna mapendekezo ya maswali ya majadiliano katika hiki kitabu, lakini waweza pendekeza maswali mengine.


Hamasisha watu mbali mbali kuchangia ikiwa ni pamoja na wanawake na vijana, wazee na watu masikini katika jamii.

Hamasisha watu wafikirie kuhusu tofauti na uhusiano baina ya mifano katika filamu na hali katika jamii.

Saidia jamii kuendeleza na kutoa mipango dhabiti kulingana na hali na vipaumbele.

Hakikisha una rekodi ya vyote vilivyosemwa, ukizingatia ahadi za maana, hatua mipango na tafakari za kuvutia.

Chukua muda kutafakari maonyesho na majadiliano ya watazamaji wako. Ni jinsi gani vitakavyoboreshwa katika uchunguzi mwingine?



# Maelezo kuhusu filamu

## Kanda 1- Vitisho na Haki

Kanda 1 - Vitisho na Haki inahusisha filamu 4 na Kuanzishwa.

Unapoweka kanda kwenye mashine ili kuonyeshwa utapata nafasi ya kuonyesha utangulizi ama uonyeshe moja kwa moja filamu bila utangulizi.

## Himaya za Maisha : Utangulizi

Meneo ya maisha ni nini? Filamu hizi ni kwa ajili ya nani? jamii inaweza vipi kutumia filamu katika vifaa vya kifurushi hiki?

Dakika kumi na nne 4

## Kwa nini kufanyika maonyesho ya 'Himaya za Maisha: Utangulizi'

Kama mwelekezaji, inafaa kutazama filamu fupi ya utangulizi kabla ya kuangalia filamu nyingine zozote katika mfululizo wa filamu hizi za himaya ya maisha. Itakusaidia kukielewa kifurushi hiki saidizi na kuamua ni filamu ipi katika zilizopo ni muhimu katika jamii.





> Kila kitu kiliharibiwa bila ruhusa, bila fidia, bila ridhaa.
>
> Silvius Kamsiu, Dayak, Indonesia

## Upokonyaji wa Ardhi Kanda 1

Jamii asili dunia nzima wanaona ardhi zao zikitishiwa na sekta za madini, viwanda na kilimo na pia miradi ya maendeleo na kuhifadhi utalii. Filamu hizi zinatazama viwango vya vitisho, wanaoongoza kufanya vitisho hivyo na pia athari za uporaji wa ardhi ulimwenguni. Katika filamu hizi tunasikia taarifa kutoka wanajamii bara la Asia, America ya kusini na Africa ambao ndio wa kwanza kupata dhoruba la athari za unyakuzi wa himaya zao. Dakika kumi na nne 14

**Kwa nini kufanyika maonyesho ya 'Upokonyaji wa Ardhi'?**
Filamu hizi zinafaa kuonyeshwa katika jamii ambazo mashamba makubwa,madini na maendeleo mengine makubwa makubwa yanafanyika ama yanaweza fanyika baadaye. Yaweza pia kufanyiwa maonyesho kwa maafisaa wa serikali, katika vyuo vikuu na umma kwa ujumla ili kuwapa mwamko kuhusu unyakuzi wa ardhi.

Tembelea tuvuti **www.lifemosaic.net/eng/tol/more/swahili-version-himaya-za-maisha/** ufahamishwe zaidi kuhusu rasilimali, takwimu na utafiti kuhusu kila aina ya hizi filamu.



“Iwapo misitu itatoweka, tamaduni zetu zitatoweka.”

Fransiskus Kaise, Malind, Papua

## Maswali ya Majadiliano

Kuna matishio gani katika himaya yako? Maendeleo gani mengine makubwa yanatokea katika eneo lako?

Ni athari gani jamii zinapata kutokana na kunyang’anywa ardhi zao?

Ni nini unachofanya kwa sasa kuzuia/kulinda ardhi yenu, ni nini waweza fanya zaidi?

## Mapendekezo Shughuli za Kufuatilia

Peleleza sekta na kampuni ambazo zinazojishughulisha kiuchumi katika maeneo yako na pia kujua ni nani amehusika kwa kuzipa sekta na kampuni hizo ruhusa za kujishughulisha.

Tembelea jamii ambazo kwa sasa zinaishi karibu na viwanda vikubwa au zinaishi karibu na migodi makubwa ya madini na ujifunze kuhusu athari wanazozipata.






> Wanasema, 'Tutaleta maendeleo, kutakuwa na hospitali na shule nyingi.' Lakini kwa ukweli si waaminifu, hizi ni ujanja wa kuwafanya wanajamii wakubali watakaloambiwa.
>
> Ramon Fogel, Paraguay

## Mbinu za Kampuni Kanda 1

Filamu hii inaelezea mbinu ambazo makampuni yanatumia ili kuwashawishi wanajamii kuwakubalia na kuwaunga mkono katika miradi yao. Na pia inaonyesha kuwa mbinu hizi zinatumika katika sekta mbalimbali duniani kote.

Wakati jamii zinapofahamu kuhusu mbinu hizi na kujitayarisha kukabiliana nazo. Wanajamii wanaweza kujipanga kwenye nafasi zao na kushikilia maamuzi yanayohusu ardhi kuhusishwa na maendeleo ya nje. Dakika kumi na nne 14





> "Jamii zinapaswa kuwa wadadisi wanapoona maendeleo kama haya yanakuja katika maeneo yao. Je yanaleta faida? Kutakuwa na athari zozote katika mazingira ama uchumi wa ndani?"

Suryati Simanjuntak, Indonesia

## Maswali ya Majadiliano

Ni nini sifa nzuri na mbaya za kushauriana na ridhaa? Ni nani mhusika?


Andaa orodha ya mbinu unazojua ambazo kampuni zinatumia kupata mashamba (Ahadi za maendeleo, hongo na ufisadi, vitishona na ukali na vinginevyo.) Kwa kila mbinu andaa orodha ya njia ya kukabiliana na mbinu hizo.

Ni mtu yupi ama taasisi gani itakayowakilisha jamii yako katika mazungumzo na watu wa nje?

Kama jamii yako inashuku ya kwamba kiongozi hawakilishi maoni ya jamii kwa upana ama ni mfisadi, ni hatua gani utakayochukua, ama ni vikwazo vipi mtakayoweka?

## Mapendekezo Shughuli za Kufuatilia

Kama kampuni imevutiwa na kuwekeza katika himaya yako, tuma wawakilishi kutoka katika jamii yako watembelee jamii zingine ambazo zina hao wawekezaji ili kujua mwenendo wao.






> "Himaya kwa mtazamo wangu ni maisha kwa ujumla."
>
> Pesr Waira Velasco Tumiña, Misak, Colombia

# Umuhimu wa Himaya Kanda 1

Ni nini faida au umuhimu wa hati-miliki ya ardhi kwa jamii asili? umiliki huu una umuhimu gani kwa mazingira na nchi kwa ujuma?
Dakika kumi na nne 9

## Kwa nini kufanyika maonyesho ya 'Umuhimu wa Himaya'?

Filamu hii inaweza kuonyeshwa kwa jamii, maafisa wa serikali na umma kwa ujumla. Hii yote ni kwa madhumuni ya kueneza ujumbe kuhusu umuhimu wa umiliki rasmi wa ardhi kwa jamii asilia, mazingira na jamii kwa ujumla.





> Tunapoweza kusimamia na kufikia misitu yetu,inadumisha mila na tamaduni zetu kwa pamoja.
>
> Yohanes Ole Turuni, Maasai, Tanzania

## Maswali ya Majadiliano

Ni nini maana ya himaya kwako na kwa jamii yako?

Jamii yako inapata faida gani kutoka kwenye himaya yako kwa maana ya kitamaduni, kiuchumi, hali ya maisha/matumizi ya kila siku, maji na kadhalika

Je, umiliki halisi, rasmi na usalama wa ardhi yenu ingeweza kuwapa faida zipi kimazingira na jamii nzima?

Je unaitunza na kuilinda vipi himaya yako?

## Mapendekezo Shughuli za Kufuatilia

Katika vikundi vidogo vidogo, orodhesha rasilimali zote amabazo himaya yenu huwapa bila malipo ambavyo vinginevyo ungenunua (kwa mfano chakula, dawa, nguzo za kujengea, vifaa vya kimila).

Jadili au onyesha kwenye ramani eneo la himaya ambalo unapatia rasilimali zingine kama maji yaliyohifadhiwa.

Tembelea tovuti **www.lifemosaic.net/eng/tol/more/swahili-version-himaya-za-maisha/** na ufahamishwe zaidi kuhusu rasilimali, takwimu na utafiti kuhusu kila aina ya filamu hizi.




"Kuwa na ardhi kubwa ya kijumuiya, tunaweza kulinda utamaduni wetu na kujiendeleza sisi wenyewe. Ni vizuri tuwe na himaya za kijumuiya."

Elias Piaguaje, Secoya, Ecuador

# Haki za Ardhi - Kanda 1

Filamu hii inaelezea na kulinganisha mikataba ya jamii katika ardhi ya umma, ardhi za kibinafsi na umiliki wa maeneo ya kijumuiya. Ilamu hii ni maalumu kwa jamii ambazo haki za ardhi bado hazijatambulika, kuwasaidia kujua ni haki gani wanazihitaji. Dakika kumi na nne 14





> “Kuna baadhi ya watu ambao wanauza sehemu za ardhi zao kwa bei ya chini kabisa. Wakati mwingine wanauza maeneo yao ili kulipia ada za shule kwa watoto wao, au kwa ajili ya kununua ng’ombe wawili kama mtaji wa kuanza biashara ya ufugaji.”
>
> Samwel Nangiria, Maasai, Tanzania

## Maswali ya Majadiliano

Je ni kwa jinsi gani mnatarajia serikali ya nchi itambue haki za jamii asilia? Ni haki zipi mnazohitaji juu ya ardhi zenu na rasili mali?

Ni nini mipaka ya himaya yenu, je eneo lenu linahusisha nini na haihusishi nini?

Ni nani anayemiliki ardhi ambayo kwa pamoja inaunda eneo lenu la mababu/himaya? Je hali hii imekuwa na mabadiliko gani kwa miongo iliyopita?


Je, ni nini jukumu la taasisi za kimila na uongozi wa kimila katika usimamizi wa himaya?

Ni kanuni zipi zinazotumika katika kuuza au kugawanya eneo lenu?

Je ni zipi faida na hasara za umiliki wa mtu mmoja mmoja na umiliki wa jumuiya kwenye haki ya ardhi.

## Mapendekezo Shughuli za Kufuatilia

Zifahamu taratibu za kisheria na hali halisi ya haki ya ardhi kwa watu asili wa nchi yako.





"Ndio, maisha yamebadilika sana. Hatutaki kuacha tamaduni zetu , lakini sisi kama vijana,tunajipata katika nja mbili, katika tamaduni na kizungu na katika tamaduni zetu wenyewe."

Alonso Martinez, Colombia

# Kanda 2 - Suluhui na Msukumo

Kanda ya pili ya suluhu na msukumo inahusisha vidio 6 za jamii asilia wakipambana kwa ajili ya ardhi yao, himaya yao na rasilimali zao. Unapopata kuonyesha filamu ya kanda hiyo pia utapata nafasi ya kuonyesha utangulizi au kuonyesha moja kwa moja filamu ya suluhu na msukumo.





“Mpango wa Maisha imezaliwa katika himaya yetu, ardhi yetu asilia, mamlaka yetu, jamii ya watu wote kwa jumla. Inashirikisha na inashikilia ndani yake nguvu zetu, udhifu wetu na fursa zetu.”

Jeremias Tunubala, Misak, Colombia

## Mpango wa Maisha Kanda 2

Misak ni jamii asilia ambao himaya yao inapatikana Cauca, Colombia. Kama jamii asili nyingi za Latin Amerika, Misak walipoteza himaya zao nyingi katika siku za ukoloni. Katika miaka ya 1970 walianza mchakato wa kurudisha mashamba yao na walifanikiwa kupata kwa urasmi haki ya ardhi zao kutoka kwa serikali . Tangu wakati huo jamii ya Misak waliendeleza  Mpango wa Maisha kama kifaa cha kuamua maendeleo kuhakikisha faida zao zitahifadhiwa kwa vizazi vijavyo. Dakika kumi na nne 23



> "Hatutaki mpango wa maendeleo, tunataka mpango wa maisha. Maisha ni nini kwetu haswa? Ni asili,lugha zetu, mila zetu na tamaduni zetu simulizi."

Liliana Muelas, Misak, Colombia

## Maswali ya Majadiliano

Maendeleo kwako ni nini na inatofautiana vipi na maana ya maendeleo inavyotumika na serikali na makampuni?

Ni njia gani unazoweza kutumia ili kuhakikisha kila mtu katika jamii anahusika katika maendeleo na kuhimarisha maono ya baadaye?

Unaweza kulinda vipi utamaduni na utambulisho wako?

Ni nini historia ya watu wako katika maeneo?

## Mapendekezo Shughuli za Kufuatilia

Tembelea maeneo yako.
Na jamii zote zilizoko, zunguka katika mipaka yote ya maeneo yako , ukijikumbusha kuhusu hadithi sehemu takatifu.

Tengeneza kikundi kinachokusanya habarina andaa orodha ya maswali yanayohusu matumaini msukuma na ujuzi na pia yanayohutajika kwa jamii. Kisha kikundi hicho kiwahoji na kukusanya mahojiano na hufahamisha jamii matokeo.

Sherehekea utamaduni wako. Panga matukio ya kitamaduni muweze kula kwa pamoja,hadithi,kosmologia,ujuzi wa kitamaduni, michezo na kadhalika. Alika jamii jirani yako na umma.




> "Tumejifunza kuwa umoja na mshikamano ni ufunguo. Hakuna mamlaka zinazoweza kukabiliana na umoja."

Noorkishili Naingisa, Maasai, Tanzania

# Wanawake mashujaa wa Ololosokwan DVD2

Wanawake asili wa Maasai Tanzania waliongoza harakati za kulinda maeneo yao.

Filamu hii ni kuhusu wanawake wenye nguvu walio ongoza harakati za haki ya ardhi kwa watu asilia. Bila indini ya wanajamii, sehemu kubwa ya ardhi ya wanajamii hao ilichukuliwa. Pindi wanawake katika jamii hiyo walipogundua kuwa jitihada za kulinda ardhi yao ilishindikana, waliamua kuchukua maamuzi mikononi mwao. Wanawake hao walitumia muamko wa kusimama, kuandamana na shinikizo la kisiasa ili kuongoza harakati katika kulinda maeneo yao. Dakika kumi na nne 15





> Serikali inazungumza kuhusu sheria na sera lakini Wamaasai tunazungumza kuhusu himaya na maisha.
>
> Kijolo Kakeya, Maasai, Tanzania

## Maswali ya Majadiliano

Uongozi unamaanisha nini kwako?Ni nini jukumu la wanawake katika uongozi katika jamii yako?

Je wanawake katika jamii yako wanachukua jukumu la kulinda maeneo? Kama sivyo, ni vikwazo vipi vinavyosababisha washishiriki na ni vipi vanavyoweza kurekebishwa?

katika hadithi hii wanawake walianzisha mwamko ili kuwapa wanawake wengine ujasiri wa kushiriki katika kulinda maeneo yao.Je ni mada gani ambayo mwamko huu unaweza kuhusisha katika jamii yako?

Katika hadithi hii wanawake walitumia aina ya mikakati tofauti tifauti(maandamano,shinikizo la kisiasa,vyombo vya habari mfumo wa kisheria na kadhalika) kulinda maeneo yao. Je ni mikkati gani yanawezekana katika haki yako na una mpango gani wa kuitekeleza?

Wanawake katika hii story wanazungumza kuhusu umoja na umiliki wa kuwa ufunguo wa mafanikio ya mapambano. Je unaweza kuhamsisha vipi amani katika jamii yako?( Kwa mfano, kupitia mwamko,muziki na nyimbo, kazi za kijumuiya kuwapa moyo ili washiriki waote na kadhalika)

## Mapendekezo Shughuli za Kufuatilia

Panga kikundi cha wamama watakao pendekeza mwamko kwa jamii

Watafutie wanawake fursa ya kuwakilisha kwenye vijiji , baraza mjadala kuhusu ardhi, siasa za ndani na kadhalika.



"Tuna hospitali yenye vifaa vya kutosha, tumeweka nishati ya jua. tumejenga shule hapa kutumia mchango uliotoka kwenye usimamizi wa misitu. Kumekua na faida hizi zote katika jamii."

Ana Centeno, Guatemala

## Hekari nusu Milioni za Matumaini Kanda 2

Kaskazini Mahariki ya Guatemala, miongoni mwa uharibifu wa kale wa Maya na misitu ya mvua, kuna msitu mkubwa dunia nzima uliotunzwa na jamii. filamu hii inaeneza habari njema na hadidhi kuhusu jinsi gani jamii asilia na jamii kwa ujumla wanavyoshirikiana kuulinda na kudumisha msitu wenye hekari nusu milioni. hili limeta faida za imaisha na watu walio mashinani. Dakika kumi na nne 12





> "Misitu ni muhimu kwetu, na tunailinda kwa maana maisha yetu yanaitegeme."
>
> Salvador García, Guatemala

## Maswali ya Majadiliano

Je ni mawazo gani ambayo jamii yako inayo kuhusu mbadala wa maendeleo ya kiuchumi?(Mbao, misitu isiyo na bidhaa za mbao, utalii na kadhalika) Utawakilisha vipi?

Je mna ujuzi gani na taratibu gani za kitamaduni ambazo kwa pamoja unasaidia kuongoza na kulinda maeneo au misitu yenu?

ACOFOP ni kikundi kinachoongozwa na jamii kuwakilisha sauti za jamii na kuwepo kwa maslahi yao. Una kikundi chochote kinacho ongozwa na jamii na wanaweza kuimarishwa vipi?

## Mapendekezo Shughuli za Kufuatilia

Fikiria kuhusu jamii na eneo lenu kulingana na nguvu zake, upungufu wake, nafasi zake na tishio zinazopata.

Kuwa na mkakati wa mbadala za kuendeleza uchumi katika jamii yako.





"Vyombo vya habari vina nguvu nyingi za kushawishi wanaofanya uamuzi, kushawishi mipango ya mashirika na wakati mwingine kuzuia maendeleo, vyombo vya habari vikipata ujumbe kutoka kwa jamii."

Samwel Nangiria, Maasai, Tanzania

# Mawasiliano Kanda 2

Filamu hii inaangalia jinsi jamii tatu kutoka Indonesia, Tanzania na Ecuador wanavyotiumia redio, mtandao, kuhusisha vyombo vya habari vya kitaifa na vya kimataifa, na pia kutumia Filamu vya mapambano yao ili kuelezea mapambano yao mashinani na duniani kote. Dakika kumi na nne 12

## Maswali ya Majadiliano

Je, ni habari au ujumbe gani muhimu inayofaa kuelezwa kwa jamii yenu?

kwa kawaida, ni njia zipi zinazotumika kueneza ujumbe kati ya jamii kwa jamii? je ni vipi njia hizi zaweza kuimarishwa?

## Mapendekezo Shughuli za Kufuatilia

Unda makundi madogo ya mawasiliano yatakayotumika kutathmini njia tofauti za kuwepo kwa mbinu ya mawasiliano inayoongozwa na jamii ili kuwasaidia kupigania na kukinga haki zao na himaya yao.

Ni nini kinachohitajika ili kuweza kuweka redio ya jamii katika himaya yenu? Nendeni mkafanye uchunguzi kuhusu redio za kijamii, zinaweza kuwepo chache karibu na jamii zenu angaliea na unakili kile mnachohitaji kukifanya ili kuwezesha kuweka kituo chenu cha redio katika eneo lenu. Jee ni vifaa gani mnavyovihitaji? Na ni aina gani ya ruhusu mtakayohitaji kuwa nayo na ni kwa gharama gani?



"Kwa sasa duniani kote kuna sheria za kimataifa zinazokulinda. Pia kuna sheria nchini mwako ambazo zinakulinda wewe kama mwananchi. Wewe ni sehemu sehemu ya jamii katika taifa lako na unaweza kutumia sheia hii kupigania haki zako."

Donald Moncayo, Ecuador

# Utumiaji wa Sheria Kanda 2

Filamu hii inaangalia kesi tatu za kisheria katika mataifa ya Indonesia, Tanzania na Paraguay ikitumia sheria za kitaifa na kimataifa. Pia inaangazia faida na hasara za kuenda kotini. Dakika kumi na nne 13

## Maswali ya Majadiliano

Je ni sheria zipi (katika wilaya, mkoa au kitaifa) zinazoadhiri jamii aidha vyema au vibaya? Je, katiba yenu ya kitaifa ina vipengele vinavyolinda haki ya jamii asilia?

Je, ni sheria ipi ya kimataifa inalinda jamii yenu? (Kama vile mkataba wa umoja wa mataifa kuhusu haki za jamii asilia au mikakati nambari 169 ya mashirika ya kimataifa ya umma). je, nchi na serikali yenu imetia sahihi mikakati yoyote ya kimataifa yanayoweza kutumika katika kulinda haki za jamii za ardhi?

Je, ni nini kati ya changamoto katika kupeleka kesi kortini? Je, kuna njia za kuepuka changamoto hizi?

Je, ni wapi mtaenda ili kupata usaidizi wa kisheria?

# Habari za Ziada

## Omba nakala Zaidi, Marejesho na Maoni

Kama utaonyesha filamu ya kwanza ya himaya za maisha utaona kuna kibahasha kinaitwa mp4s. Kibahasha hiki kina filamu zenye muonekano wa kiwango cha chini ambazo unaweza kuweka katika kadi yako ta kumbukumbu ama kifaa chochote kinachoweza kucheza mp4.

Filamu zote pia zinapatikana kwenye mtandao **www.lifemosaic.net/eng/tol/more/swahili-version-himaya-za-maisha/**katika lugha tofauti.

Tafadhali wasiliana na info@lifemosaic.net ili uweze kuomba nakala zaidi. Wasiliana na LifeMosaic kuwaeleza jinsi ulivyotumia filamu zao na hatua zilizochukuliwa na jamii yako kama matokeo. Mafundisho hayo yatatumika kusaidia jamii zingine na kutumika katika warsha zingine hapo baadae.

## Nani alitengeneza Himaya za Maisha?

Himaya za Maisha yalianzishwa na LifeMosaic wakishirikiana na AMAN na zaidi ya makundi 20 ya jamii kutoka maeneo ya jirani. LifeMosaic ni shirika lisilo la kiserikali linalosaidia jamii asili kulinda haki zao, maeneo na tamaduni zao. LifeMosaic inatoa elimu ya bure kwa jamii na inawezesha usambazaji mpana wa rasilimali hizi.


Tembelea tovuti
**www.lifemosaic.net/eng/tol/more/swahili-version-himaya-za-maisha/**
ufahamishwe zaidi kuhusu rasilimali, takwimu na utafiti kuhusu kila aina ya hizi filamu.



**Himaya za Maisha**

Kitabu hiki kinaambatana kanda ya Himaya za Maisha.

**Kitabu hiki kinaambatana kan Imefadhiliwa na :**
CLUA,
Ford Foundation,
Network for Social Change,
Margaret Hayman Charitable Trust,
Waterloo Foundation,
Bertha Foundation,
The Christensen Fund.

Yaliyomo katika kitabu hiki hakiwakilishi maoni ya wafadhili.

Kitabu hiki kinaweza kunakiliwa na kusambazwa bure
kwa matumizi ya jamii asilia pamoja na mashirika yaliyosaidia jamii hizo.

# Himaya za Maisha